

OFISI YA RAIS - TAMISEMI

HALMASHAURI YA WILAYA YA WANGING'OMBE

SHULE YA SEKONDARI THOMAS NYIMBO,
S.L.P 204,

MAKAMBAKO.

TAREHE 12.12.2020

Kumb Na:-TNSS/JOINST/2020/01

Jina La Mwanafunzi

S. L. P **UHAMBULE.**

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI THOMAS NYIMBO. WILAYA YA WANGING'OMBE MWAKA 2021

1.UTANGULIZI.

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha Kwanza mwaka **2021**, Shule ya **Sekondari Thomas Nyimbo**.Shule hii ipo kijiji cha Igelango kata ya Uhambule, Tarafa ya Wanging'ombe Wilaya ya Wanging'ombe.

Muhula wa Masomo utanza Tarehe 11/01/2021.Unatakiwa kuripoti Shuleni kuanzia Tarehe **10/01/2021**,na mwisho wa kuripoti ni Tarehe **17/01/2021**

2.MAMBO YA KUZINGATIA.

- Sare za shule

Sare ya shule hii ni

➤ **Wavulana**

- ❖ Suruali mbili, za damu ya mzee zenye marinda.(**zisiwe za kubana**)
- ❖ Mashati meupe mawili mikono mifupi
- ❖ Soksi nyeusi za kutosha
- ❖ Sweta blue shingo ya V
- ❖ Viatu vyeusi vya ngozi vyenye visigino vifupi na Vya kamba pea mbili(visiwe choma)
- ❖ Track suit ya rangi ya bluu kwa ajili ya kujikinga na baridi jioni (isiyobana)
- ❖ Aje na nguo za ndani za kutosha.
- ❖ Aje na Fulana(Singland) zisizopungua 2 nyeupe za kuvaa ndani
- ❖ Vifaa vya Usafi ni, ndoo 1, Fyekeo 1, na fagio la chelewa 1
- ❖ Aje na nguo za Michezo ambazo ni, bukta ya rangi Nyekundu, T- Shirt Nyekundu na raba

➤ **Wasichana**

- ❖ Suruali mbili za damu ya mzee .(**zisiwe za kubana**)
- ❖ Kigauni cha Kitambaa cheupe cha solo chenye marinda,Shingo duara (Mbili)Mchoro upo karatasi ya nyuma
- ❖ Track suit nyeusi kwa ajili ya kujikinga na baridi jioni(isiyobana)
- ❖ Sweta ya blue yenye shingo ya V
- ❖ Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba visivyo na visigino virefu
- ❖ Soksi nyeupe za kutosha
- ❖ Gauni la kushindia rangi Dark blue (Mshono liwe la solo)
- ❖ Aje na nguo za ndani za kutosha na Taulo za Kike (Pedi)
- ❖ Aje na nguo za Michezo ambazo ni, bukta ya Bluu, raba na T- Shirt Ya Bluu
- ❖ Vifaa vya Usafi ni, ndoo 1, jembe 1, na fagio la chelewa 1

➤ **WOTE**

- ❖ Daftari kubwa(kaunta quire 2) 10
- ❖ Kalamu za Bluu/Nyeusi za kutosha,Kalamu za risasi,Mkebe, Rula na Kamusi(Dictionary)
- ❖ Jalada moja kwa ajili ya kutunzia taarifa zake(File)

3.Sheria na Kanuni za Shule

Shule inaendeshwa kwa Mujibu wa sheria ya Elimu Na 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na 10 ya Mwaka 1995.Aidha,inazingatia miongozo yote iliyotolewa na Wizara ya Elimu,Sayansi,Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya Rais-TAMISEMI yenye jukumu la Usimamizi na Uendeshaji wa Elimu

3.1.Hivyo unatakiwa Kuzingatia mambo ya Msingi ambayo yatafuatiliwa muda wote uwapo shuleni,Kama ifuatavyo

- a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- b) Marufuku kwenda na kandambli eneo lolote la chakula
- c) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima
- d) Kushiliki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
- e) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazo pewa .
- f) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- g) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
- h) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapo takiwa (Huruhusiwi kuja na Nguo zisizotakiwa shuleni)
- i) Unatakiwa Kuomba ruhusa au kutoa taarifa wakati wowote unapokuwa na shida
- j) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote : na
- k) Kutunza mali za umma.
- l) Huruhusiwi kuja na nguo za nyumbani

3.2. Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha **kufukuzwa au kusimamishwa Shule.**

- a) Wizi
- b) Utoro
- c) Kujihusisha na Mapenzi ukiwa Shuleni au Nyumbani huku ukiwa Mwanafunzi
- d) Uasherati na ushoga.
- e) Ubakaji
- f) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile, uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika .
- g) Kupigana au kupiga .
- h) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma .
- i) Kudharau Bendera ya Taifa,Wimbo wa Taifa na Alama nyingine za Taifa.
- j) Kuwa mjamzito /kupata mimba.
- k) Kuoia au kuolewa.
- l) Kutoa mimba.
- m) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiliki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
- n) Kukataa adhabu kwa makusudi.
- o) kuwa na simu ya mkononi maeneo ya shule

Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa Shuleni na Mwanafunzi.

- a) **Medical Examination form**, Ambayo itajazwa na Mganga mkuu wa Hospitali ya Serikali. fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakapo ripoti Shuleni
- b) Fomu ya maendeleo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai
- c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

4.MAHITAJI YA HOSTEL (DAHARIA)

Kila mwanafunzi aje na vifaa/vitu vifuatavyo

- Godoro la kulalia futi $2\frac{1}{2} \times 6$
- Blanketi ya kujifunika
- Mashuka mawili ya rangi ya **Bluu**(Wavulana) na **Pink**(Wasichana)
- Mto na foronya lake
- Sabuni, mswaki, dawa ya meno, kandambili kwa ajili ya usafi. Bila kusahau Pakiti ya wembe
- Chandarua (neti) kwa ajili ya kujizuia na mbu.
- Tochi
- Vifaa vya kulia chakula kikombe, bakuli 1, sahani1, na kijiko 1.
- Kidumu cha kuwekea maji ya kunywa.

Michango ya Chakula

- Mahindi debe 10 kwa mwaka
- Maharage debe 02 kwa mwaka
- Mchele debe 01 kwa mwaka
- Fedha ya chakula/hosteli Tshs 110,000/= kwa mwaka (Pesa hii ilipwe Awamu Tatu),Januari-Machi Tsh 30,000/= Aprili-Juni Tsh 50,000/= na Julai-Oktoba Tsh 30,000/=
- **Pesa ya kitanda** Tshs 46,000/= kwa kila mwanafunzi itatolewa mara moja tu.
- **NB: Fedha zote zitumwe kwenye akaunti ya shule ya sekondari Thomas Nyimbo (NMB) Na 60601000036.**(Andika Jina la Mwanafunzi na Pesa hiyo ni ya nini,Mfano,Chakula au Kitanda) Bank Pay Slip(BPS) iletwe Shuleni
- **Ujenzi wa Miundombinu ya Shule:** Wanafunzi wanaotoka Ndani ya Kata ya Uhambule ni **Tsh 10,000/=** Na Wanafunzi Wanaotoka Nje ya Kata ya Uhambule ni **Tsh 20,000/=**(Hii ni Makubaliano ya Kikao cha Kamati ya Maendeleo ya Kata ya Uhambule na Kata Ya Udonja Walichokaa Tarehe 04/11/2019) Fedha iingizwe kwenye Akaunti namba **63210002096 Thomas Nyimbo Sekondari. NMB Wanging'ombe**

Tafadhari soma kwa makini maelezo /maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

Karibu sana katika shule hii

.....
Mwl.L.E.Mbwilo
Mkuu Wa Shule
(075-5526845)

HALMASHAURI YA WILAYA YA WANGING'OMBE
SHULE YA SEKONDARI THOMAS NYIMBO
S. L. P. 204, MAKAMBAKO.
FOMU YA KUKUBALI NAFASI YA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA.

SEHEMUA: (IJAZWE NA MWANAFUNZI MWENYEWE)

Mimi Nimesoma na kuelewa masharti yote na sheria za shule. **Nayakubali/Siyakubali** kwa hiyo **Ninaipokea /Siipokei** nafasi hii niliyopewa. Ninaahidi kuwa nitazingatia masharti na sheria za shule zote na nitakuwa mtiifu mpaka kumaliza kidato cha Nne.

Sahihi ya mwanafunzi Tarehe

SEHEMU B: (IJAZWE NA MZAZI /MLEZI)

MimiMzazi wa**Ninakubali/sikubali**, nafasi aliyopewa mtoto wangu . Ninaahidi kutimiza mahitaji yote ya shule na kusaidiana na walimu kumlea kielimu na kitabia.

Sahihi ya mzazi / mlezi Tarehe

.....
Mkuu wa Shule

WANGING'OMBE DISTRICT COUNCIL
THOMAS NYIMBO SECONDARY SCHOOL
P. O. BOX 204, MAKAMBAKO

To
The Medical Officer,

.....
.....
.....

Re REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION:

Please kindly examine (Name) to determine His/Her Physical
and Mental fitness for pursuing Secondary School studies.

.....
Head of School

1. Eyesight
2. Hearing
3. Speech
4. Limbs
5. Leprosy
6. Epilepsy
7. Cardiac Diseases
8. Rheumatism
9. Venereal Diseases
10. Pregnancy (for Girls)
11. General Comments

.....

Signature*Date*.....

Official Stamp

N.B. Any disease **detected** should be treated

